

Nifanye Nini Ili Niokolewe?

Nifanye nini ili niokolewe?

Mtu akisema na aseme kama mausia ya Mungu, (1 Peter 4:11).

1. Watu Wote Wana Wajibu Wa Kuokoka.

Wote wametenda dhambi (Warumi 3:23; 1 Yohana 1:10). Mshahara au adhabu ya dhambi ni mauti (Warumi 6:23; Ezekieli 18:4). Mungu katika neema yake anataka watu wote waokolewe (2 Petro 3:9; Yohana 3:16). Kwa hiyo ikiwa twataka tupokee neema ya Mungu iwezayo kutuokoa yatupasa kufuata masharti ya Yesu.

2. Katika Agano Jipya Kuna Mambo Ambayo Yameunganika Kuhusu Wokovu.

Neema (Tit. 2:11; 3:3-8; Efe. 2:8-10).

Imani (Mdo. 16:31; Mk. 16:15-16).

Toba (Mdo. 17:30-31; Lk. 24:47).

Kukiri (Mt. 10:32-33; Rum. 10:9-10).

Ubatizo kwa ondoleo au msamaha wa dhambi (Mdo. 2:37-38; 22:16, 3:19).

Uaminifu wa maisha mapya (Rum. 6:3-16; 1 Thes. 1:8-9; Ufu.2:10).

3. “Je, Nimepungukiwa Kitu Gani?”

Watu wengine wameyatii maagizo ya Kristo kuhusu toba. Watu wengine hawajamsikia Kristo. Maagizo ya bwana kuhusu wokovu yanapaswa yaeleweke kufuatana na yale ambayo mtu hajayafanya. Kwa hiyo mtu inampasa kujuua, afanye nini ili aokoke.

4. Neno la Mungu Linaleza Wazi Mtu Afanye Nini Ili Aokoke.

Mtu aliyeisikia injili inampasa kumwamini Kristo (Mdo. 16:31). Kama hafanyi hivyo atakufa katika dhambi zake (Yn. 8:24). Mtu aliyeamini katika Kristo anaambiwa atubu (Mdo. 2:38). Kama sivyo ataangamia (Lk. 13:3-5).

Akiamini na kutubu anahitaji kumkiri Kristo Mdo. 8:36-39; Rum. 10:9-10, kama hafanyi hivyo atakataliwa na Kristo siku ya hukumu (Mt. 10:32-33).

Wote ambao wameamini, wametubu, na kumkiri Kristo ni lazima wabatizwe kwa kupata ondoleo la dhambi (hebu “ni lazima” katika Mdo. 9:6 tena soma Mdo. 22:1-16; Rum. 6:3-4; Gal. 3:26, 27, 29). Kama mtu hafanyi hivyo hawezi kuurithi ufalme wa Mungu (Yn. 3:3-5).

Wale ambao wamebatizwa, wanaamriwa kuishi maisha ya uaminifu (maisha ya utauwa) Kol. 2:12-14; 3:1-6; 1 Kor. 15:58; Lk. 9:62). Ikiwa mtu hafanyi hivyo ataanguka kutoka katika neema ya Mungu (Ebr. 3:12; Gal. 5:4; 2 Pet. 2:20-22).

Wale ambao walibatizwa na kuwa Waristo halafu wakaanguka kutoka kwenye uaminifu wao wameamriwa kurudia kwa Mungu kwa njia ya kutubu na kwa maombi (Mdo. 8:22; Lk. 15:11-32; 1 Yn. 1:7-10) kama mtu hafanyi hivyo atatupwa nje (1 Kor. 9:27; Ufu. 2:4-5).

RAFIKI YANGU MPENDWA?

Ikiwa mtu ameokolewa au amepotea jambo la lazima ni kupata uzima au mauti.

Swali hili “nifanye nini ili niokolewe” limeulizwa mara nyingi sana, na ni katika Biblia peke yake tunamoweza kupata jibu la uzima wetu kwa Mungu sisi tukiwa washiriki wa Kanisa la Kristo twajibiidisha kila tuwezavyo kuzifuata kwa uaminifu Sheria za Mungu kusudi tupate baraka za neema yake (Ebr. 5:9; 2 Thes. 1:7). Lolote likipungukiwa katika uaminifu wa mmoja

Kwa haraka audhurie. Imani, toba, kumkili Kristo, ubatizo kwa ondoleo la dhambi, uaminifu katika ibada kanisani.

Ikiwa kati ya haya yako uliyopungukiwa katika kumwamini Mungu, tunakusahi uyarekebishe haraka mawazo yako, na tuko tayari kukusaidia kwa njia yo yote.

Tutakavyoweza, kila mara utakuta makaribisho yanakungojea kwenye ibada zetu.

www.kanisalakristo.com